TANGAZO LA SERIKALI Na. 672 la tarehe 2/8/2024

SHERIA YA USIMAMIZI NA USHURU WA BIDHAA,
(SURA YA 147)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 128)*

AMRI YA MSAMAHA WA USHURU WA BIDHAA KWA MAGARI ISHIRINI NA TATU YANAYOINGIZWA NCHINI NA OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA KWA AJILI YA USIMAMIZI NA UENDESHAJI WA MRADI WA TACTIC NA MSIMBAZI YA MWAKA 2024

Jina

**1.** Amri hii itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Ushuru wa Bidhaa kwa Magari Ishirini na Tatu yanayoingizwa Nchini na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa ajili ya Usimamizi na Uendeshaji wa Mradi wa TACTIC na Msimbazi ya Mwaka 2024 na itachukuliwa kuwa ilianza kutumika kuanzia tarehe 12 Juni, 2024

Msamaha

**2.** Kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika aya ya 3 na masharti mengine yoyote yanayoweza kuainishwa na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, kiasi chote cha ushuru wa bidhaa kinachotakiwa kulipwa kuhusiana na magari Ishirini na Tatu yaliyoainishwa katika Jedwali la Amri hii, yanayoingizwa au kununuliwa ndani ya nchi, kabla ya kibali kupitia forodha kwa niaba ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ili kutumiwa kipekee katika Uendeshaji wa Mradi wa TACTIC na Msimbazi kimesamehewa.

Masharti

**3.** Msamaha wa kodi unaotolewa chini ya Amri hii utakoma na ushuru utapaswa kulipwa kana kwamba

Amri hii ya msamaha haikuwa imetolewa, iwapo magari husika yatatumika kwa madhumuni mengine au kuhamishwa, kuuzwa au kuondokana nayo kwa namna yoyote kwenda kwa mtu mwingine asiyestahili kufaidika na manufaa yanayofanana na hayo au yaliyotolewa chini ya Amri hii.

Ukomo

**4.** Msamaha uliotolewa chini ya Amri hii utafikia ukomo tarehe 11 Januari, 2025

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

| Na. | maelezo | Nambari ya Chassis | Nambari ya Injini | Idadi | Mahali liliponunuliwa/ Kuagizwa ndani |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Toyota Land Cruiser 300-Series Diesel, 5 Door, 7-Seater | JTMAACBJ204073386, JTMAACBJ404076788, JTMAACBJ204074053, JTMAACBJ504065766, JTMAACBJ004067375, JTMAACBJ504067310 | F33A-0078199, F33A-0082051, F33A-0079094, F33A-0070767, F33A-0072333, F33A-0072276. | 6 | Limeagizwa |
| 2 | Toyota Land Cruiser Prado TXL, Turbo Diesel, 5 Door, 7-Seater | JTEBR9FJ00K335665, JTEBR9FJ60K335685, JTEBR9FJ50K335693, JTEBR9FJ80K335705, JTEBR9FJ50K334886, JTEBR9FJ30K335028, JTEBR9FJ70K335078, JTEBR9FJ40K334275, JTEBR9FJ50K336575, JTEBR9FJ50K336794, JTEBR9FJ20K336882, TEBR9FJXOK337231, TEBR9FJ90K337284, TEBR9FJ20K337367, TEBR9FJ60K337016, TEBR9FJ90K336362, TEBR9FJ60K336481, | 1GD9257956, 1GD9257760, 1GD9257772, 1GD9258154, 1GD9255204, 1GD9255488, 1GD9255777, 1GD9253000, 1GD9261663, 1GD9262129, 1GD9262276, 1GD9263876, 1GD9264221, 1GD9264416, 1GD9263271, 1GD9260552, 1GD9261098, | 17 | Limeagizwa |

Dodoma,
25 Julai, 2024

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU,
*Waziri wa Fedha*